

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

06

URAIA NA MAADILI

Muda: Saa 1:30

20 Novemba 2019.

Maelekezo

1. Mtihani huu una sehemu A na B zenyé jumla ya maswali **sita (6)**
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.
3. Sehemu A ina alama **ishirini na sita (26)** na sehemu B ina alama **ishirini na nne (24)**

SEHEMU A (Alama 26)

1. Jibu vipengele (i) – (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika kisanduku.
 - (i) Unapaswa kufanya nini unapoishi na watu wenyé tabia zisizokubalika katika jamii?
 - A. Kuwakimbia bila kuwashauri C. Kupigana nao hadi wabadilike
 - B. Kuwavumilia na kuwashauri D. Kuwatolea maneno makali []
 - (ii) Njia ipi inaweza kutumika katika kutatua changamoto zinazokukabili?
 - A. Kuzikubali na kuweka malengo
 - B. Kuwa ombaomba na kutaka ushauri
 - C. Kuchoka na kukata tamaa
 - D. Kuweka malengo na kuyaacha []
 - (iii) Lipi kati ya matendo yafuatayo yanaonesha tabia ya ustahimilivu?
 - A. Kudadisi bila kuchoka na kupata jibu
 - B. Kufanya kazi kwa bidii na kupumzika sana
 - C. Kufanya kazi haraka haraka
 - D. Kufanya kazi polepole []
 - (iv) Kuhimili vikwazo katika maisha kunatuwezesha kufikia.
 - A matatizo yetu ya kila siku C. ugumu wa maisha
 - B heshima yetu. D. malengo yetu []
 - (v) Hali ya kujiamini na kutarajia mafanikio katika jambo fulani hujulikana kama
 - A Udadisi C Mtazamo chanya.
 - B Changamoto. D Uvumilivu. []

2. Jibu kipengele (i) - (iv) kwa kuoanisha maelezo kuhusu alama za Taifa katika **Fungu A** na alama za Taifa katika **Fungu B**. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

Fungu A	Herufi	Fungu B.
(i) Huonesha utajiri wa mali asili ya nchi yetu.	[]	A. Bendera ya taifa
(ii) Humutika katika barua za kiofisi na machapisho ya serikali.	[]	B. Jembe na nyundo
(iii) Huashiria uhuru wa nchi yetu.	[]	C. Wimbo wa taifa
(iv) Huwakilisha vifaa vinavyotumika kuendeleza taifa.	[]	D. Nembo ya taifa. E. Fedha za Tanzania F. Pembe za ndovu

3. Chagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano na liandike katika sehemu iliyoachwa wazi.
- (i) Kitendo cha mtoto kushiriki katika maamuzi huonyesha _____ (wajibu wa mtoto, haki ya mtoto, kukomaa kwa mtoto)
 - (ii) Ili watoto wapate msaada mara wanapohitaji wanatakiwa wawe: .(wanafiki, wakweli, wazembe)
 - (iii) Lipi kati ya yafuatayo ni wajibu wa mtoto? _____ (kupendwa, kupata chakula, kufanya kazi rahisi)
 - (iv) Kitendo cha mtu kufanya kazi aliyopangiwa huitwa _____ (wajibu, haki, uaminifu)

SEHEMU B (Alama 24)

4. Jibu vipengele (i) – (v) kwa kuweka alama ya **vema** (✓) kuonesha kama zana zilizowekwa kwenye jedwali ni za asili au siyo za asili. Namba moja imetolewa **kama mfano**.

Zana	Zana za Asili	Zana zisizo za Asili
(i) Gitaa		✓
(ii) Manyanga		
(iii) Kinanda		
(iv) Filimbi		
(v) Tarumbeta		

5. Chunguza kwa makini picha ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.



Maswali:

- (i) Ni kitendo gani kinaoneshwa katika picha? _____
 - (ii) Unafikiri kwanini mtu huyu katika picha anafanya kitendo hiki? _____
 - (iii) Ni hasara gani inayosababishwa na kitendo
kinachofanyika katika picha? _____
 - (iv) Pendekeza njia mojawapo inayoweza kutumika kulinda
na kutunza mazingira ya eneo liliooneshwa kwenye picha
-
6. Soma kwa makini kifungu cha habari kifuatacho kisha
jibu maswali yanayofuata.

*Vyanzo vya maji ni muhimu katika maisha yetu. Mfano wa vyanzo
vya maji ni mito, maziwa, bahari, mabwawa, visima, mvua na
chemichemi.*

*Tunapaswa kuvilinda vyanzo hivi vya maji. Tunaweza kuvilinda
vyanzo vya maji kwa kutokata miti ovyo kandokando ya vyanzo
vya maji, kupanda miti,*

kutojisaidia au kutupa taka kwenye vyanzo vya maji.

*Maji yanatumika kwa kunywa, kupikia, kuoshea, kuoga,
kusafisha na kumwagilia mazao. Ni wajibu wa jamii nzima
kuvilinda vyanzo vya maji.*

Maswali:

- (i) Kulingana na kifungu hiki cha habari, mito, maziwa, bahari, mabwawa na mvua huitwa _____
- (ii) Ni nani anawajibika kulinda vyanzo vya maji? _____
- (iii) Tunawezaje kuvitunza vyanzo vya maji? _____
- (iv) Tunatumia maji kwa shughuli zipi? _____